

GRADE 3 END TERM 3 MARCH 2022
KISWAHILI

JINA

Nambari ya mwanafunzi Jinsia: Mvulana Msichana

Jina la shule Msimbo wa shule

Mwalimu ajaze jedwali hili baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi

Sehemu ya	Alama	Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio
1 Kusikiliza na kuzungumza					
2 Kusoma					
3 Sarufi					
4 Kuandika					

SEHEMU YA 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

1. Mwalimu hufanya kazi gani shuleni?
2. Mtu anayefanya kazi ya kupika huitwaje?
3. Toa maelezo kumhusu seremala.
4. Anayeendesha gari ndiye nani?
5. Daktari hufanya kazi gani?

SEHEMU YA 2: KUSOMA

Zoezi la 1: Kusoma kwa sauti.

Soma hadithi hii kwa sauti.

Nampenda sana mama yangu kwa sababu ananipenda. Yeye ni mama mpole na karimu. Akiwa na pesa, yeye hunitembeza katika sehemu mbali mbali. Iwapo hana pesa, sisi hukaa nyumbani. Kila tuendapo sokoni, mama huninunulia nguo mpya. Kila Jumamosi, yeye hunipeleka kanisani. Katika likizo iliyopita, mama alinipeleka kuizuru mbuga ya Nairobi ambapo niliwaona wanyama kama vile pundamilia, twiga na simba. Ameniahidi baiskeli iwapo matokeo yangu yatakuwa bora kuliko muhula uliopita.

Alama 10

Zoezi la 2: Kusoma kwa ufahamu

Soma hadithi hii na ujibu maswali

Sokoni ni mahali ambapo bidhaa mbalimbali huuzwa na kununuliwa. Watu wengi wanaoishi mijini hawana mashamba humo ambapo wanaweza kuvuna mboga na nafaka. Wanapohitaji bidhaa hizi, huwabidi kuzinunua sokoni. Licha ya vyakula, vitu vingine kama vile vyombo na fanicha huweza pia kuuzwa masokoni. Katika masoko mengi, maeneo hugawanywa kulingana na kinachouzwa pale. Mtaani mwetu, Jumamosi ndiyo siku rasmi ya soko.

11. Sokoni ni mahali ambapo _____ huuzwa na kununuliwa.
12. Wanaoishi mijini huweza kuvuna _____ na _____
13. Watu wa mijini wanapohitaji bidhaa kama mahindi, wao huzinunua wapi?

14. Licha ya vyakula, _____ na _____ pia huuzwa sokoni.
15. Siku rasmi ya sokoni katika mtaa wa mwandishi ni _____

SEHEMU YA 3: SARUFI

Tumia "ndani ya" au "nje ya" kwa usahihi.

16. Mti mrefu ulimea _____ nyumba.
17. Samaki huogelea _____ maji.
18. Mama alitia maji _____ sufuria.
19. Wanafunzi wamekaa _____ darasa wakiota jua.
20. Nywele huota _____ ya kichwa. (nyuma, juu, chini)
21. Ng'ombe wamejilaza _____ ya mti (chini, katikati, juu)
22. Ndege mkubwa alitua _____ ya tawi (juu, chini, ndani)

Ziandike sentensi hizi katika wakati ujao.

23. Alipokea chanjo ya ugonjwa wa Korona. _____
24. Wanacheza ngoma za kitamaduni. _____
25. Alivalia mavazi ya kupendeza. _____

SEHEMU YA 4: KUANDIKA

Tumia maneno uliyopewa kujazia mapengo

ng'ombe nyasi nyumbani maziwa minne

- Mnyama nimpendaye ni _____ 26. Mnyama huyo huishi _____ 27. Yeye ana
masikio mawili, pembe mbili na miguu _____. Mnyama mwenyewe hula _____
na kutupa _____ 28. tunayokunywa na kupikia chai. _____ 29